**Malen Pre and Primary School**
Aspire for Excellence

Kiboga, Mvuti, Dar es Salaam
Head Teacher: **0692485846**, Director: **0768185858**

## MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE (SCHOOL JOINING INSTRUCTION) 2026

Ninafuraha kukujulisha ya kwamba mwanao amechaguliwa kujiunga katika shule yetu ya Malen. Tunakukaribisha katika familia yetu ya Malen.

Nikuhakikishie kuwa elimu ya mwanao ni kipaumbele chetu na ni wajibu wetu kutoa elimu iliyokamilika na kujitosheleza. Kupitia jitihada zetu madhubuti na ushirikiano kutoka kwako, tunaimani wanafunzi wetu watakua na kusitawi katika kila nyanja kimaadili, kimwili, kiroho na kiakili ikimuwezesha kupata maarifa na ujuzi utakao msaidia kuwa mwanafunzi wa kujitegemea.

### MISINGI YA MAADILI NA MAJUKUMU.

1. **Kuhusu Malen.**
   Shule ya awali na ya Msingi ya Malen ni shule inayoendeshwa kwa misingi ya Imani ya Waadventista Wasabato ambayo kusudi lake ni kutoa elimu itakayomkuza mtoto kiroho, kiakili, kimwili na kijamii.
   Lengo kuu la shule ya **Awali na Msingi Malen** na nia yake ni kufuzu kwa viwango vya juu kielimu na kiroho na kukuza jamii yenye maadili na kutoa watoto na wafanyakazi wenye nidhamu ya hali ya juu.
2. **Maadili yetu ya Msingi.**
   Kilele cha mafanikio kitafikiwa endapo jamii yote ya **Malen**, wakiwemo, walimu, wazazi na wanafunzi watavuta kwa pamoja huku wakizingatia maadili, misingi na majukumu yafuatayo:
   - **i.** Mungu ndiye chanzo cha maarifa yote ya mwanadamu.
   - **ii.** Tunaheshimu Biblia kama kitabu kitakatifu tunakitumia kama rejeleo la kufundishia au kutoa elimu ya dini kwa wanafunzi wetu.
   - **iii.** **Mazingira mazuri ya kujifunzia huanza nyumbani ambapo wazazi kama walimu wa kwanza wanapaswa kupandikiza maoni mazuri kwa wanafunzi wetu.**
   - **iv.** Kufanya kazi kama timu (**mzazi na shule**) kutatuwezesha kufikia lengo letu kabisa.
   - **v.** Upendo na heshima kati ya wazazi na shule ni lazima kwa uendeshaji mzuri wa mifumo yetu.
   - **vi.** Uwazi, ukweli na uaminifu ni nguzo ya ubora wetu.

**vii.** Watoto ni wa thamani sana kwa Mungu, kwa hivyo jukumu letu ni kwamba, kuhakikisha tunasogeza mioyo yao kwa Mungu bila kuchoka.

**viii.** Kuwalinda watoto wetu dhidi ya ulimwengu ulioharibiwa ni wajibu wetu, hivyo kila mmoja wetu awajibika, katika kujenga tabia njema katika akili za wanafunzi wetu.

3. **Wajibu wa mzazi.**

Kama mzazi unawajibika kwa mambo yafuatayo ili kusaidia shule ya **Malen** kufikia malengo ya juu:

**i.** Kulipa ada ya shule kwa ukamilifu na kwa wakati kama inavyoelekezwa kwenye **Jedwali la mpangilio wa ulipaji Ada**.

**ii.** Kusaidia kukuza mipango na malengo ya kitaaluma iliyopangwa na shule.

**iii.** Kusaidia wanafunzi kuelewa sheria za shule na kanuni ili tuweze kuwa na wanafunzi wanaojitambua.

**iv.** Kumpatia mtoto mahitaji muhimu ya kumfanya awe na mazingira mazuri ya kujifunzia.

**v.** Kumlea mtoto na falsafa kamili, kwa kumjenga kiakili, kimwili, kiroho na kijamii.

**vi.** **Kufuatilia na kuhakikisha kuwa mtoto wako anamaliza kwa unadhifu kazi za nyumbani alizopewa shuleni.ZINGATIA,kama mwanafunzi hajamaliza kazi za nyumbani hatachukuliwa na gari la shule mpaka atakapomaliza kazi zote.**

**vii.** Kuwasaidie watoto kutunza vitabu vyao vya mazoezi.

**viii.** Kuimarisha maadili na tabia njema ambayo mtoto hufundishwa shuleni.

**Mzazi/Mlezi atakayekuja kwenye MAZINGIRA ya shule akiwa amevaa mavazi yasiyo na maadili mafupi na yaliyobana hataruhusiwa kuingia ndani ya geti.Hivyo zingatia Mavazi yenye staha ujapo shuleni.**

**ix.** Kuhakikisha kuwa mtoto anahudhuria siku zote za shule bila kukosa isipokuwa kuna dharura, tafadhali ifahamishe shule kwa simu au kwa barua ikiwa mtoto wako hajafika shuleni kwasababu yoyote isipokuwa ya **ADA.** Na kama anaumwa toa taarifa mapema na siku akija shuleni aje na cheti cha hospital. **Akikaa nyumbani kwa muda wa wiki moja bila taarifa yeyote atakuwa amejiondoa na mzazi utatakiwa uje uchukuwe uhamisho wake.**

x. Ikiwa mtoto anakuja shuleni na dawa, tafadhali hakikisha kuna barua inayoelezea kipimo na nyakati zinazohitajika dawa hizo kutumiwa (bila barua ya maelekezo mtoto hatapatiwa dawa).

xi. **Kila Jumapili ya kwanza ya mwezi ni siku ya wazazi kuwatembelea watoto (visiting day),Muda wakuwatembelea watoto ni kuanzia 6:00 mchana hadi saa 10:00 jioni.**

xii. **Siku ya kuja kuwatembelea watoto hatutaruhusu chakula chochote kutoka nje,Vyakula vyote vitapatikana hapo shuleni kwa gharama ya kawaida.**

xiii. Hakikisha mwanao yupo katika muonekano mzuri (**msafi**) anapotoka nyumbani kuja shuleni. Hii ni miongoni mwa usafi wa sare za shule, nguo za ndani, nywele, kucha, meno n.k pia mwanafunzi anapaswa kuvaa sare ilioelekezwa kikamilifu, **HATUTAMPOKEA MTOTO KAMA HAJAVAA SARE YA SHULE.**

xiv. Tafadhali zingatia tarehe za kufungua na kufunga shule.Mzazi hakikisha mwanafunzi amerudi shuleni kwa wakati,kama hatashindwa kurudi kwa wakati bila sababu za msingi atachukuliwa hatua kali za kinidhamu.

xv. Wanafunzi hawaruhusiwi kuleta chakula, vinywaji au pesa yoyote shuleni.

xvi. **Mzazi kama unachangamoto yoyote tunakuomba uonane na uongozi,ni jambo baya kuongea changamoto ya shule mbele ya mtoto/mbele za watu wasiohusika.**

xvii. Ukilipa ada hakikisha umeleta **PAYSLIP** shuleni au utume kwa Whatsapp kwaajili ya kukatiwa risiti ya shule kabla ya kufungua shule ili kuepuka usumbufu.

Siku ya kufungua shule sio siku ya kujadili ulipaji wa **ADA** lipa kwa wakati maana pasipo kulipa kiwango chote mtoto hatapokelewa kabisa.

xviii. **Kama kuna changamoto inayohusu shule sio vema mzazi kuongelea mbele ya mtoto kwa sababu hiyo inaweza kumfanya mtoto kudharau shule ikamfanya kushuka kitaaluma na kinidhamu pia.**

xix. Hakikisha begi la mwanao ni safi na linafunga zipu vizuri kuepuka upotevu wa madaftari ovyo.

xx. Kuepukana na upotevu wa nguo, tunaomba uweke lebo / alama yakuonekana katika nguo zote. Nguo ambazo hazijawekwa lebo **HAZITAPOKELEWA.**

xxi. Endapo mwanafunzi ataharibu kifaa cha shule, mzazi au mlezi atawajibika katika malipo yote ya gharama ya uharibufu huo.

4. **Wajibu wa wanafunzi:**

i. Mtoto anatakiwa aongee **KIINGEREZA** wakati wote akiwa shuleni na akiwa kwenye gari la shule. Mtoto wa darasa la awali atalazimika kusoma kwa miaka mitatu (**Baby class, Middle class na Senior class**).

ii. **Mtoto asipopata 90% kwa Awali na 70% kwa shule ya Msingi atarudia Darasa. Hivyo ni wajibu wa kila mmoja wetu kufanya nafasi yake kwa uaminifu ili kumsaidia mtoto apate wastani unaohitajika na shule.**

iii. Wapende na uwaheshimu watu wote bila kujali umri, jinsia au hadhi.

iv. Epuka matumizi ya lugha mbaya (matusi), uonevu na ugomvi dhidi ya wengine na ikiwa mwanafunzi atafanya hivyo mzazi / mlezi wa mtoto atapewa taarifa na hatua za kinidhamu zitachukuliwa.

v. Hakikisha mazingira ya shule yanawekwa safi wakati wote.

vi. **Ni marufuku mwanafunzi kukaa kwenye kitanda cha mwanafunzi mwingine, na ikibainika hatua za kinidhamu zitachukuliwa.**

vii. Wakati wa kuabudu ni wakati muhimu kwa Malen kwa kila mtu kuhudhuria, kwahiyo hakuna mwanafunzi anayeruhusiwa kuchelewa au kukosa kipindi chochote cha Ibada.

viii. Shule hairuhusu nguo fupi,Nguo zinazobana na mapambo kama hereni na cheni za shingoni, upakaji wa kucha rangi, Usukaji wa rasta nk.

ix. Kelele hairuhusiwi wakati wa masomo.

x. Kama mtoto ana tabia inayojirudiarudia isiyoendana na maadili yetu tutamuita mzazi kwa onyo la kwanza akiendelea tutamruhusu amtafutie mwanaye shule nyingine.

xi. Stationary zote zinapatikana shuleni, kwahiyo haturuhusu mtoto kuja na ufutio, penseli n.k

xii. **Kipindi cha mvua tunaomba ushirikiano, tunaomba umlete sehemu inayofikika isiyokuwa na MADIMBWI.**

xiii. Unakumbushwa tena, kuwa **Shule ya Awali na ya Msingi ya Malen** ni shule inayoendeshwa kwa misingi ya Imani ya Waadventista Wasabato ambayo kusudi lake ni kutoa elimu itakayomkuza mtoto kiroho, kiakili, kimwili na kijamii.

xiv. Endapo mwanafunzi ataharibu kifaa cha shule, mzazi au mlezi atawajibika katika malipo yote ya gharama ya uharibufu huo.

xv. Mwanafunzi anatakiwa atunze madaftari ya kazi ya shule na kazi ya nyumbani pamoja na Diary. **NB: Kama daftari limenyofolewa karatasi na jaladio**

**limetolewa au amepoteza, mzazi atawajibika kulipa daftari kwa Tsh 5,000/- na jaladio 2,000/-,Kalamu sh 1000/- na kama mtoto amepoteza Diary mzazi atanunua kwa gharama ya Tsh 15,000/-**

**xvi.** Usafi na unadhifu ni lazima kila wakati kwa **Malen**. Vaa sare sahihi kwa siku kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| **JUMATATU** | **Gauni / Sketi + blauzi**<br>**Suruali / Kaptula + Shati**<br>**Viatu vyeusi vya Ngozi + Soksi nyeupe + Tie** |
| **JUMANNE** | **Red trucksuit + Red tshirt**<br>**Raba nyeupe + soksi nyeupe** |
| **JUMATANO** | **Njano na nyeusi suti**<br>**Viatu vyeusi vya ngozi +soksi nyeusi** |
| **ALHAMISI** | **Suruali/skirt/kaptula+Blue tshirt+soksi nyeupe** |
| **IJUMAA** | **Maroon Trucksuit + Dark blue tshirt**<br>**Raba nyeupe + soksi nyeupe** |

**Angalizo**.

- Kumbuka kujaza kwa usahihi na kuirudisha **APPLICATION FORM** kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti,mtoto hatapokelewa pasipo form hiyo.

**MEDICAL CHECKUP.**

- Kila mwanafunzi anahitajika kufanya ukaguzi wa afya **(medical checkup)** kutoka katika kituo cha afya kinachoaminika. Fomu ya afya imeambatanishwa kukupatia muongozo juu ya swala zima la ukaguzi huo. Fomu hii itakusanywa kwa mwalimu atakayehusika siku ya kuripoti mtoto shuleni.Kwa **watoto wa bweni waje na bima ya afya.**
- Na mwanafunzi wa Bweni atapewa ruhusu kwaajili ya checkup kama itamlazimu kwa siku ya Jumatano au Alhamisi tu.